

Malengo ya Mradi

- Kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya zinazomlenga mtumiaji.
- Kuboresha uwezo wa watu binafsi katika jamii mbalimbali kufuata tabia njema za kiafya.
- Kuboresha mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora za afya.

Mfadhili wa Mradi

Msaada kutoka kwa watu wa Marekani

Mtekelezaji Mkuu wa Mradi

Deloitte Consulting Limited

Watekelezaji Wenza wa Mradi

Management and Development for Health na T-MARC Tanzania

Watekelezaji Shirikishi

Mamlaka za serikali za mitaa, vituo vya afya, mashirika ya huduma za jamii, mashirika ya msingi ya jamii na mashirika ya misingi ya imani za kidini



Anuani

Deloitte Consulting Limited
USAID Afya Yangu Southern
3rd Floor, ARiS House,
Plot No. 152, Haile Selassie Road,
P O Box 1559, Dar es Salaam – Tanzania
www.deloitte.com



USAID Afya Yangu Southern



USAID Afya Yangu Southern

USAID Afya Yangu Kanda ya kusini



Maisha yenye afya bora na jamii zinazostawi

Kuhusu mradi

Mradi wa USAID Afya Yangu Kanda ya Kusini (2021-2026) unalenga kusaidiana na Serikali ya Tanzania kutoa huduma bora jumuishi za matunzo, matibabu, na kuzuia maambukizi ya VVU na kifua kikuu ambazo zitaboresha matokeo chanya ya afya, hasa kwa vijana na watoto.

Mradi unakusudia kuongeza mahitaji na matumizi jumuishi ya huduma bora za VVU na kifua kikuu katika mikoa ya Iringa, Lindi, Morogoro, Mtwara, Njombe, na Ruvuma kwa kuboresha upatikanaji wa huduma bora katika vituo vyote vya afya na jamii zote zinazozunguka maeneo hayo, ili kukuza tabia chanya kwa watazania kupata huduma za afya na kuimarisha mazingira ya jumla ya sera ya utoaji wa huduma za VVU na kifua kikuu.



Maono

Maisha yenye afya bora na jamii zinazostawi.

Dhima

Kuongeza mahitaji na matumizi jumuishi ya ubora wa matunzo, matibabu, na kuzuia VVU na kifua kikuu, hasa kwa vijana na watoto, kupitia mbinu ya kina inayozingatia mteja na kupata matokeo bora ya afya.



Huduma za Afya Zinazotolewa na Mradi

VVU na kifua kikuu ikiambatana na huduma jumuishi za uzazi wa mpango na jinsia.

Mikoa ya Mradi

Iringa, Lindi, Morogoro, Mtwara, Njombe na Ruvuma.

Mfumo wa Utoaji Huduma

Mradi huu unatoa msaada wa kiufundi na nyenzo na msaada wa kiutawala na usimamizi kwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Serikali ya Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia mamlaka za serikali za mitaa, ngazi ya mikoa na wilaya, vituo vya afya vya umma na binafsi, na asasi za kijamii (mashirika ya huduma za jamii na mashirika ya kidini) ili kuongeza uwezo wao wa kusimamia na kutoa huduma bora za VVU na Kifua Kikuu ndani ya sekta ya umma na vituo vya afya vinavyohusiana na imani.

Mradi huu pia unaimarisha utoaji wa huduma za afya katika jamii kwa kuunganisha na kuboresha uhusiano kati ya jamii na vituo vya afya.

